

PENNSYLVANIA

*ni jimbo la msingi lililofungwa
katika suala la upigaji kura*



JIMBO LILILOFUNGWA KWA KURA YA MCHUJO NI UPI?

Katika jimbo lililofungwa kwa Kura ya Mchujo, mpiga kura **anaweza tu kupiga kura kwa wagombezi wa chama cha kisiasa ambacho mpiga kura ameandikishwa nacho.**

Katika Uchaguzi Kuu wapiga kura wote, bila kujali chama wameandikishwa nacho, wanaruhusiwa kupiga kura kwa wagombezi wote wanaoshiriki kwenye uchaguzi.

JE IKIWA NIMEANDIKISHWA NA CHAMA CHA TATU AU SINA CHAMA?

Ikiwa mpiga kura hana ufuasi wa chama chochote, kumaanisha hawajaandikishwa na chama chochote, hawataona wagombezi kwenye karatasi cha Kura ya Mchujo. Kura ya Mchujo ni kwa ajili ya kila chama kuamua wagombezi wao wa mwisho kwa Uchaguzi Mkuu. Ni wanachama pekee wa hicho chama ndio wanaweza kuamua ni mgombezi gani wa mwisho atawawakilisha katika Uchaguzi Mkuu.

Ikiwa mpiga kura ameandikishwa na chama cha tatu, wataona tu chaguzi za wagombezi kama chama hicho inashirikisha mgombezi kwenye mwaka huo wa uchaguzi. Ni muhimu kuzingatia, sio vyama vyote vya tatu hushirikisha wagombezi kila mwaka au katika wilaya zote.

Wapiga kura wote, bila kujali ufuasi wa vyama, wanaweza kupigia kura maswali ya kura na mashindano yasiyogemea upande wowote, kama nafasi zilizoachwa wazi na chaguzi maalum, kwenye Kura ya Mchujo. Ni muhimu kuzingatia kuwa sio kila mwaka kutakuwa na maswali ya kura na chaguzi maalum.

Katika Uchaguzi Kuu wapiga kura wote, bila kujali chama wameandikishwa au kutoandikishwa nacho, wanaruhusiwa kupiga kura kwa wagombezi wote wanaoshiriki kwenye uchaguzi.

SINA UHAKIKA NI CHAMA GANI NIMESAJILIWA NACHO

Unaweza kuangalia hali yako ya usajili katika:

[HTTPS://VOTE.PA.GOV/STATUS](https://vote.pa.gov/status)

Daima kuna chaguo la kubadilisha chama ambacho umesajiliwa nacho wakati wowote katika mwaka. Wapiga kura lazima wasasishe usajili wao kabla ya siku ya mwisho ya usajili wa wapigakura ujao ili kuona mabadiliko yanaonekana katika kura zao.

TAREHE YA MWISHO YA KUBADILISHA CHAMA CHAKO

Ikiwa ungependa kusasisha ufuasi wako wa chama, itabidi usasishe usajili wako wa wapigakura. Tarehe ya mwisho ya kujisajili kupiga kura ni **Mei 1, 2023**. Unaweza kujisajili kupiga kura katika ofisi ya uchaguzi ya kaunti, kwa kutuma barua, au kwenye mtandao katika:

[HTTPS://VOTE.PA.GOV/REGISTER](https://vote.pa.gov/register)